**TATHMINI YA PAMOJA YA KAUNTI YA NANDI KASKAZINI NA NANDI YA KATI 2016**
**KISWAHILI**
**INSHA**
**102/1**
**KARATASI LA KWANZA**

1. Swali la lazima.
   Andika barua kwa mhariri wa gazeti la Mulika kuhusu **vyanzo vya ujauzito kwa wanafunzi wa kike nchini.**
2. Eleza jinsi udanganyifu katika mitihani utaathiri maisha ya kizazi kijacho.
3. Uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti.
4. Andika insha ambayo utamaliza kwa:
   ……………….Aha! Kumbe muungwana akivuliwa nguo huchutama! Sitahisahau siku hiyo kwani sijawahi kufedheheka maishani kama nilivyoaibika.

**TATHMINI YA PAMOJA YA KAUNTI YA NANDI KASKAZINI NA NANDI YA KATI 2016**
**KISWAHILI**
**102/2**
**LUGHA**
**KARATASI LA PILI**

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

Lugha inaweza kuelezwa kwa jumla kuwa ni mfumo wa mawasiliano.Haiyamkiniki_kwa mtu yeyote kueleza chanzo au kiini cha lugha na sote tunakubalina kuwa matumizi yake yameanza tangu kuumbwa kwa binadamu kwani ni vigumu kukisia kuwepo kwa jamii ya watu bila lugha ya mawasiliano yoyote ile.

Katika taifa lolote,huwapo na lugha moja au hata zaidi ya moja ambayo huwa ndicho chombo zatika cha mawasiliano ya taifa katika nyanja za:elimu maandishi,siasa na biashara.Kwa mfano mataifa ya Kanada hutumia lugha mbili kwa usawa kama lugha za taifa na za kikazi.Maana ya lugha ya taifa ni lugha moja ambayo huteuliwa kutumika katika shughuli zote za taifa hasa katika nchi yenye lugha nyingi za kikabila.Lugha ya taifa ni muhimu sana kwa maisha na maendeleo ya taifa lolote lile.Lugha hii huwa ndiyo kiungo cha kueneza umoja na uelewano miongoni mwa jamii nyingi tofauti na huwa kama kitambulisho kwao kwa kuwa wao ni ndugu wa jamii moja kubwa,yaani taifa lao.

Kenya ni mfano mzuri wa taifa lenye lugha nyingi zinazozidi 40 za vikundi vidogo vidogo vya kikabila.Hapo kabla ya miaka mia moja hivi iliyopita kila kimojawapo cha vikundi hivi kilijitambulisha kama kabila huru.Baada ya kuja kwa serikali ya kikoloni na hasa baada ya Kenya kujinyakulia uhuru,haja ya kuunganisha raia wote chini ya taifa moja lenye uongozi na shabaha moja ilikuwa ndilo jambo lililozingatiwa sana.Kwa hivyo utamaduni wa taifa Kenya ni mchanganyiko wa tamaduni za watu wengi wenye mila,desturi,imani na itikadi tofauti.Utamaduni humaanisha jumla ya amali na tabia za watu wa jamii fulani.Amali hizi zinafungamanisha fikira,ustaarabu,mila,taasisi na sanaa za aina zote za jamii inayohusika.

Ili kujieneza na kujiimarisha,taifa huhitaji chombo hicho kuwasiliana na kuwaunganisha watu wake wenye asili mbalimbali. Chombo hicho huwa ni lugha ambayo siyo tu kwamba ni sehemu ya utamaduni wa jamii bali pia ni njia muhimu sana ya kutawanyia na kustawishia ule utamaduni.

Katika taifa lenye lugha nyingi kama Kenya kwa mfano,lugha ya taifa inayozungumzwa na kueleweka na baadhi kubwa ya raia ambayo imekiuka mipaka na tofauti za kikabila ni njia muhimu sana ya kueneza maongozi ya taifa na kuleta ufahamikiano bora kote nchini.Kama

zilivyo taasisi kama wimbo wa taifa,bendera ya taifa au bunge la taifa, lugha ya taifa ndicho kielelezo cha taifa lolote lile.Lugha kama hiyo huvunja na hukomesha hisia za kibinafsi na kikabila na badala yake kuunda moyo wa uaminifu wa kitaifa.

Zaidi ya kuwa chombo cha mawasiliano,lugha ni kielelezo cha fikira na hisia za binadamu.Lugha ya watu fulani haituelezi tu ujuzi au maarifa yao bali pia mtazamo wao kimaisha,falsafa na mawazo yao.Kwa ufupi lugha hutufahamisha namna akili za watu waizungumzayo ile lugha zinavyofikiri na kufanya maazimio.Lugha ni sehemu ya utamaduni wa taifa tulimozaliwa na lazima lugha hiyo ifunzwe katika muktadha wa maisha ya jamii ihusikayo.Utamaduni wa jamii havitenganiki na lugha yake.

**Maswali**

(a) Huku ukirejelea kifungu, eleza fasiri na chanzo cha lugha. (alama 2)
(b) Tofautisha baina ya lugha ya taifa na lugha ya kikazi. (alama 4)
(c) Kwa nini lugha ya taifa huhitajika sana katika nchi kama Kenya. (alama 4)

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call 0720502479

(d) Eleza kazi **nne** kuu zinazotekelezwa na lugha ya taifa. (alama 2)

(e) Eleza maana ya mafungu yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa: (alama 3)

(i) Amali na tabia za watu:………………………………………………………………………..

(ii) Muktadha wa maisha ya jamii:…………………………………………………………………….

(iii) Haiyamkiniki:……………………..……………………………………………………………..

2. **UFUPISHO: (ALAMA 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Je, mtazamo hasi ni nini? Huwa na athari gani kwa binadamu hadi iwe sababu ya kuangaziwa katika safu hii? Mtazamo hasi ni kukata tama, kutamauka kuhusu hali, mtu au jambo fulani. Ni hisia ya kutotaka kushiriki wala kuhusishwa na jambo au hali fulani. Mtazamo huu ndio huwafanya wanafunzi wengi kuchukia au kudunisha baadhi ya masomo na walimu wanaowafundisha. Licha ya wengi kuwa na mtazamo huu, kwa kweli huwa hawatambui. Asilimia kubwa ya wanaotambua hutatizika kujikwambua kutoka katika hali hii.

Inakadiriwa kwamba mtu wa wastani huwa na takriban mawazo elfu sitini ya kibinafsi kwa kila saa 24. asilimia 95 ya fikra hizi huwa sawa na za siku iliyotangulia, na asilimia 80 ya fikra hizi zilizorudiwa huwa hasi.

Isitoshe, fikra hizi nyingi hutokea bila mtu mwenyewe kutambua na huwa mazoea. Hii ina maana kwamba watu wengi hawana ufahamu wa athari za fikra hizi maishani mwao. Katika makala haya tunaangazia vyanzo vya mitazamo hasi na suluhu.

Mwanzo kabisa ni imani potovu. Hiki ndicho chanzo kikuu cha mtazamo hasi. Kushikilia imani potovu kuhusu maisha pamoja na matukio fulani maishani hujenga mtazamo hasi. Unayaona maisha kwa macho ya imani zako na iwapo imani hizo ni potovu, basi hutayathamini maisha yako. Ili kukabiliana na hali hii, sharti kwanza ubadili imani yako. Uamini kwamba mabadiliko yanaweza kutokea na uchukue hatua ya kuanzisha mabadiliko hayo maishani mwako. Unahitaji kuepuka fikra hasi zinazoambatana na maisha yako ya awali na kulitathmini kila tukio maishani kama tukio huru; lisilo na uhusiano na yaliyowahi kukutamausha.

Kujikwamua kutoka katika imani duni unahitaji kuibuka na idadi kubwa ya imani chanya kuliko zilizo hasi kuhusu hali mahsusi. Baada ya hilo, zikabili imani zako potovu moja baada ya nyingine huku ukijiuliza endapo imani hizo ni kweli na endapo zina mashiko, tumia dakika tano hivi kila siku kushadidia fikira chanya inayokinzana na ile inayokudidimiza. Ukifanya hivi kwa takriban siku thelathini imani yako itaanza kuchuku mkondo unaofaa.

Familia au rafiki anaweza kuwa kikwazo. Pasipo kufahamu familia yako na rafiki unaoandamana nao huathiri pakubwa hisia zako. Wakiwa na mtazamo hasi huweza kukushawishi ukaanza kuhisi wanavyohisi na kuyaona mambo kwa mtazamo wao. Kukabiliana na hali wapaswa kudhibiti hisa zako.

Tawala namna unavyohisi na kukabiliana na hali mbalimbali bila kuathiriwa na wandani hawa. Epuka wandani wa aina hii kadri inavyowezekana, ikiwezekana, jitenge nao ili ujifunze kuwa na uhuru wa kufanya maamuzi yako binafsi bila kuathiriwa nao.

Unapaswa kupunguza ushirika hata na jamaa zako wanaokuingiza katika hali ya kutamauka. Punguza muda wa kukaa nao hasa wanapogeuka mkondo huu wa kukukatiza tamaa.

Mazingira hasi ni kizingiti kingine. Pengine huoni ukuruba baina ya maisha yako na wazingira unamokulia au unamokaa. Ukweli ni kwamba, huenda umedumu katika mazingira hayo na kuyazoea hata ukafikiri huwezi kukayabadilisha. Kadri unavyohisi huna uwezo wa kuyabadilisha ndivyo unajizamisha zaidi katika mtazamo hasi. Ili kukabiliana na hali hii, unahitaji kuelewa kwamba fikra zako au za watangulizi wako ndizo zilikuingiza katika mazingira haya. Kwa hivyo unapaswa kubadili mkondo wa fikra zako na uanza kujaribu mazoezi ambayo umekuwa ukiyaona kama usiyoyaweza. Hatua kwa hatua, utagundua panapo jitihada na uelekezi unaofaa kwamba mazoezi hayo yamekuwa mepesi na hivyo kukuhakikishia kuyabadilisha mazingira yako.

Hali zisizoridhisha ni wakati unapojikuta ukilalamika jinsi ulivyokerwa na hali Fulani, hii ndiyo sababu hasa ya kuwa na mtazamo hasi kuhusu hali hizo. Inaweza kukuwa vigumu kulikubali hili lakini kadri utakavyokubali mapema ndivyo utakavyoboresha maisha yako mapema. Kulalamika tu ndiko kutakudumisha katika hali zisizokuridhisha. Ili uyabadilishe maisha yako sharti ukome kulalamika na kuanza kujikwamua toka kwenye hali hizo.

Katika kufanikisha jambo lolote jema sharti viwepo vizingiti njiani. Mtendaji wa jambo lolote jema liwalo ana jukumu la kuibuka na mikakati mwafaka ya kuvikabili vizingiti hivi ili afanikishe ndoto yake. Hii ndiyo sababu unapaswa kuchukua hatua kutokea sasa ili kupanga na kutekeleza mikakati itakayoipindua mtazamo wako hasi uwe chanya. Kwa jinsi hii utayabadilisha maisha yako yawe ya kuridhisha zaidi na kuwa kielelezo kwa wengi waliotamaushwa na mitizamo hasi.

**Maswali**

(a) Fupisha ujumbe wa aya **nne** za mwanzo kwa maneno 80. (alama 7, 1 ya mtiririko)

(b) Kwa kurejelea aya mbili za mwisho, fupisha ujumbe kwa maneno 70. (alama 6, 1 ya mtiririko)

3. **MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

For more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call 0720502479

a) (i) Taja sauti zozote **mbili** zinazotamkiwa kwenya kaakaa gumu. (alama 1)
(ii) Eleza maana ya kirai. (alama 1)
(iii) Onyesha aina ya virai katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Mwanafunzi mzuri husoma ndani ya darasa.

b) Andika sentensi hii upya bila kubadilisha maana ukitumia "O" rejeshi. (alama 2)
Mwanafunzi alitumwa nyumbani juzi na hajapata karo hadi leo.

c) Tumia kiwakilishi cha nafsi huru (nafsi ya pili wingi) katika sentensi. (alama 2)

d) Eleza matumizi ya "na" katika sentensi ifuatayo.
Simba aliuawa na wawindaji haramu nasi tukawaripoti. (alama 2)

e) Weka vitenzi hivi katika hali ya kuamrisha wingi. (alama 2)
(i) -nywa
(ii) Tubu

f) Andika ngeli za nomino zifuatazo. (alama 2)
(i) Uwele
(ii) Vita

g) Kanusha
Mwanafunzi ambaye amefika ametuzwa. (alama 2)

h) Changanua kwa kutumia mchoro wa matawi.
Mvuvi hodari alifurahi alipofanikiwa kuvua jodari.

i) Eleza matumizi moja moja ya viwakifishi vifuatavyo. (alama 3)
(i) Mshazari:…………………………………………………………………………………………
(ii) Parandesi…………………………………………………………………………………………
(iii) Ritifaa…………………………………………………………………………………………

j) Andika katika ukubwa.
Mke wa mzee huyu hupenda watoto sana.

k) Tunga sentensi **moja** kutofautisha 'thibiti' na 'dhibiti.' (alama 2)

l) Geuza sentensi hii hadi usemi wa taarifa: (alama 3)
"sitakuja shuleni kesho," mwalimu mkuu akasema, "nitaenda kuhudhuria mkutano Mombasa.:

m) Huku ukitumia mifano, tofautisha sentensi ambatano na sentensi changamano. (alama 4)

n) Ainisha mofimu katika neno: (alama 2)
Walichimba

o) Kwa kutumia mifano, tofautisha kati ya kishazi huru na kishazi tegemezi. (alama 2)

p) Eleza maana **mbili** zinazojitokeza kwenye sentensi hii. (alama 2)
Wale wamekuja kutuliza.

4. **ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

a) Eleza juhudi zozote **tano** za serikali ya Kenya katika kukuza Kiswahili. (alama 5)

b) Taja na ueleze pingamizi zozote **tano** zinazokwamiza juhudi za kukuza Kiswahili. (alama 4)

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call 0720502479